



Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 SEPTEMBER, 2024 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBER, 2024

1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 SEPTEMBER, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilidhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika. Hali hii ilisukuma sehemu ya ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi katika maeneo yaliyopo kaskazini mwa nchi (baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria). Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa Bahari ya Hindi lilikuwa la juu kuliko lile la eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusini mwa Madagascar). Hali hii iliimarisha upepo wa bahari wenye unyevunyevu kutoka kusini mashariki kuelekea eneo la pwani ya nchi yetu na maeneo jirani.

1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 SEPTEMBER, 2024

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua na ngurumo katika maeneo machache ya ukanda wa ziwa Victoria na mvua nyepesi katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki. Pia, vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa vilijitokeza katika maeneo ya ukanda wa pwani na maziwa makuu.

2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBER, 2024

2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBER, 2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendele kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusukuma sehemu ya ukanda mvua (ITCZ) kuelekea kusini hadi katika maeneo yaliyopo kaskazini mwa nchi (baadhi ya maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria). Joto la bahari katika eneo la magharibi wa Bahari ya Hindi (pwani ya Africa Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu kuliko lile la eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuimarisha upepo wa bahari wenye unyevunyevu kutoka kusini mashariki kuelekea eneo la pwani ya nchi yetu na maeneo jirani.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 11-20 SEPTEMBER, 2024

Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):

Mvua na ngurumo za radi vinatarajiwa katika maeneo machache.

Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro): Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba): Mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): Mvua nyepesi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Hali ya ukavu inatarajiwa.

Imetolewa na;

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz